



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA  
BODI YA USIMAMIZI WA STAKABADHI ZA GHALA



TANGAZO KWA UMMA

Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) ni taasisi chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara iliyoundwa kwa **Sheria Namba 10 ya Mwaka 2005** na Marekebisho **Kifungu cha 4 Sura ya 339 R.E. 2016**. Bodi imepewa majukumu chini ya Kifungu 5 (a-j) cha Sheria hiyo ikiwemo kutoa leseni kwa Waendesa Ghala, Meneja Dhamana na Wakaguzi wa Ghala.

Bodi inawatangazia wadau wote wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kuwa; kwa kuzingatia Sheria ya Stakabadhi za Ghala **Kifungu 70A(1)** uhamishaji umiliki wowote wa Stakabadhi za Ghala (mauzo) chini ya ghala zinazotekeleza Mfumo wa Stakabadhi za Ghala utafanyika kuititia majukwaa yaliyopewa leseni au kuruhusiwa kwa kuzingatia Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana.

Hivyo, Waendesa Ghala wote wanaelekezwa kutoa bidhaa ghalani kwa wanunuzi ambaa pamoja na nyaraka nyingine kusheria, watawasilisha vibali ya kutoa bidhaa vilivytolewa na Jukwaa la Mauzo liilosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ambapo kwa sasa ni Soko la Bidhaa Tanzania (TMX).

Mwendesa Ghala ambaye atatoa bidhaa kwa mnunuzi ambaye hajazingatia utaratibu huu atakuwa amekiuka utaratibu na hatua kali zitachukuliwa kwa wahusika wote

Imetolewa,

MKURUGENZI MTENDAJI  
BODI YA USIMAMIZI WA STAKABADHI ZA GHALA  
DODOMA

6 Mei 2024